**HALMASHAURI YA KALIUA**
**KATA YA KASHISHI**
**SHULE YA MSINGI KASHISHI**
**MTIHANI WA KUMALIZA MUHULA WA PILI NOVEMBA 2025**
**SOMO: URAIA NA MAADILI DARASA: VI**

**JINA LA MWANAFUNZI** ______________________________________________

**SEHEMU A: (*Alama* 20)**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi na uijaze kwenye sehemu ulizopewa.
   i. Mahakama ni mhimili wa dola unaohusiana na kazi zifuatazo isipokuwa __________________ [ ]
   A. Kupokea mashitaka B. Kutunga sheria C. Kusikiliza maelezo D. Kutafsiri sheria E. Kubaini tatizo
   ii. Nani ana wajibu wa kulinda rasilimali za Taifa?____________ [ ]
   A. Mhimili wa dola B. Askari wa wanyama pori C. Jeshi la polisi D. Kila mwananchi E. Jeshi la wananchi
   iii. Jukumu lipi linaweza kutekelezwa na mtoto katika mazingira ya nyumbani?________ [ ]
   A. Kutafuta chakula cha familia B. Kulinda familia C. Kufanya usafi wa mazingira D. Kulipa Ankara za umeme E. Kununua nguo za familia
   iv. Kitendo kipi kinaweza kuhatarisha usalama barabarani?____________ [ ]
   A. Kuendesha baiskeli pembezoni mwa barabara B. Kuvuka sehemu ya kivukomilia C. Kutembea upande wa kulia wa barabara D. Kutembea upande wa kushoto wa barabara E. Kuvuka barabara kupitia daraja la juu [ ]
   v. Matumizi ya lugha isiyofaa na kutohudhuria vipindi vya masomo shuleni ni baadhi ya makosa ya kinidhamu kwa wanafunzi. Yapi ni madhara yatokanayo na makosa hayo?_______________ [ ]
   A. Kushuka kwa morali ya kujifunza B. Kushuka kwa morali ya kufundisha kwa walimu C. Kushuka kwa viwango vya taaluma D. Kukwamisha mbinu za ufundishaji shuleni E. Kushindwa kupata mahitaji ya shule [ ]
   vi. Neno lipi linatumika kuelezea mamlaka au amri zilizowekwa ili kulinda na kuhakikisha jambo fulani linafanyika bila kujali, kupendwa au kutokupendwa na watu?___________ [ ]
   A. Maelekezo B. Taratibu C. Muktadha D. Sheria E. Mwongozo
   vii. Tabia ipi huoneshwa na mwanafunzi anayeweza kubainisha vipaumbele katika kufanya uamuzi sahihi? [ ]
   A. Kujitambua B. Kujithamini C. Kujiamini D. Kujijali E. Kujipenda
   viii. Kitendo cha mwanafunzi kuzingatia na kutekeleza taratibu zinazoongoza mchakato wa kujifunza kinaitwaje?__________________ [ ]
   A. Kutii kanuni za mwalimu wa darasa B. Kutii kanuni za familia C. Kutii sheria na kanuni za shule D. Kutii kanuni za viranja wa shule E. Kutii kanuni za jamii
   ix. Kundi lipi sio la watu wenye mahitaji maalumu katika jamii?_________ [ ]
   A. Vijana wenye nguvu B. Watu wenye ulemavu wa kusikia C. Watoto wenye ulemavu wa kusikia na kuona D. Watu wenye ulemavu wa ngozi E. Watu wenye ulemavu wa akili
   x. Chombo kinachozuia na kupambana na rushwa huitwa ____________ [ ]
   A. TAMWA B. FAO C. UNICEF D. ILO E. TAKUKURU
2. Oanisha maneno yaliyo katika orodha “A” na dhana zake katika orodha “B” kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika mabano uliyopewa.

| Orodha “A” | Majibu | Orodha “B” |
|---|---|---|
| i. Hewa ya ukaa | [ ] | A. Hujumuisha vitu vyote vinzvyomzunguka mwanadamu akiwemo binadamu mwenyewe |
| ii. Mazingira | [ ] | B. Husababisha watu kujihusisha na shughuli mbalimbali zinazoharibu mazingira |
| iii. Maliasili | [ ] | C. Huwaunganisha watu wa tamaduni tofauti |
| iv. Urejelezi | [ ] | D. Huchangia ongezeko la joto duniani |

| | | |
|---|---|---|
| v. Lugha | [ ] | E. Zoezi la kubadilidsha taka kuwa bidhaa mpya ili ziweze kutumika tena |
| | | F. Kumomonyoka kwa maadili |
| | | G. Kupinga rushwa na ufisadi katika jamii yetu |

3. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku na kuliandika katika nafasi uliyopewa.

| |
|---|
| Ubaguzi wa kijinsia,Kumi,Tanganyika na Zanzibar,Jaji mkuu,Makamu wa Rais,Kenya na Uganda,Rais |

i. Jamuhuri ya muungano wa Tanzania ni muungano wa nchi mbili ambazo ni______________________________
ii. Rais huapishwa na nani? _______________________________
iii. Waziri mkuu wa Muungano wa Tanzania huteuliwa na nani?__________________
iv. Sensa ya watu na makazi nchini Tanzania hufanyika kila baada ya miaka____________________________
v. Kitendo cha kufanya matendo yasiyofaa kwa mtu mwenye jinsia tofauti huitwa__________________________

**SEHEMU B: (*Alama* 20)**

4. Zifuatazo ni aina kuu tano za mahakama hapa Tanzania. Panga kwa kuonesha mpangilio sahihi wa ngazi za mahakama kwa kuanza na ngazi ndogo Kwenda ngazi kubwa kwa kuzipa herufi A-E
   i Mahakama ya hakimu mkazi { }
   ii Mahakama ya Rufaa { }
   iii Mahakama ya wilaya { }
   iv Mahakama kuu { }
   v Mahakama ya mwanzo { }

5.ndika jibu katika sehemu zilizoachwa wazi

i. Jambo linalomlazimu mtu kulifanya au kulitimiza huitwa _____________
ii. Ni alama ipi ya Taifa inaonesha kuwa nchi ni huru_____________
iii. Bainisha sababu mbili zinazofanya ukeketaji kukatazwa katika jamii;
   (a) ________________________________
   (b) _______________________________
iv. Bainisha viashiria viwili vya utandawazi nchini Tanzania'
   (a) ________________________________
   (b) _________________________________
v. Taja faida mbili za wimbo wa Taifa;
   (a) __________________________________ (b) ______________________________________

**SEHEMU C: (*Alama* 10)**

5. Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho kasha jibu kipengele (i) – (v) kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi ulizopewa.

Mtamaa ni kijiji kilichopo kandokando ya mto Ndurumo. Miaka mingi iliyopita kijiji hiki kilikuwa na hali mbaya ya ukame kwa sababu watu wake waliharibu mazingira. Wanakijiji walikata miti hovyo kwa shughuli za ujenzi, ufugaji, uwindaji, kilimo, uvuvi, kutengeneza samani, nishati ya mkaa na kuni. Mazingira ya kijiji yalibadilika sana na maisha ya watu yalikuwa magumu kwani joto liliongezeka. Mazao yalikauka na mifugo kukosa afya. Pia baadhi ya vyanzo vya maji ya mto Ndurumo vilivyopo katika mlima Sekenke vilikauka. Siku moja mwenyekiti wa kijiji hicho aliitisha mkutano wa dharura kwa wananchi wote ili kujadili hali ya ukame iliyojitokeza kijijini kwao. Baada ya majadiliano wananchi walikubaliana kuthamini na kutunza mazingira yao ili kuepukana na ukame. Waliafikiana kupanda miti maeneo yote ya wazi na kwenye vyanzo vya maji. Vile vile, kutunza na kuweka sheria ndogondogo zitakazosaidia uhifadhi wa miti ya asili iliyopo kijijini hapo. Miaka michache baadae, kijiji cha Mtamaa kilikuwa na miti mingi ya asili na ya kupandwa. Mvua za kutosha zilinyesha katika misimu yote na mto Ndurumo ulitiririsha maji ya kutosha kwa shughuli za kilimo na ufugaji

kijijini hapo na katika vijiji vya jirani. Pia maeneo ya kulisha mifugo yakawa na majani ya kutosha. Hali hiyo iliwawezesha wanakijiji wa kijiji cha Mtamaa kuvuna mazao yanayotosha kwa chakula na biashara.

**MASWALI**

i. Ni tatizo gani lilikikumba kijiji cha Mtamaa kwa miaka mingi? ________________________

ii. Kwa nini mto Ndurumo ni muhimu kwa wakazi wa kijiji cha Mtamaa? ________________________

iii. Ni shughuli gani zilisababisha wananchi wa kijiji cha Mtamaa kukata miti ovyo? ________________

iv. Je, baada ya majadiliano, wananchi wa kijiji cha Mtamaa walikubaliana kufanya nini? ______________

v. Mlima Sekenke una faida gani kwa maisha ya wananchi wa kijiji cha Mtamaa? ________________